JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OWM – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI
SHULE YA SEKONDARI MKONGO

Phone: +255 784 227 470
+255 783 330061

S.L.P 40,
IKWIRIRI-RUFIJI,
TANZANIA

YAH: KUJIUNGA NA SHULE

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao ……
Amechaguliwa kujiunga kidato cha TANO katika shule ya Sekondari Mkongo, Tunampongeza kwa mafanikio hayo. Shule itafunguliwa mwanzoni mwa mwezi July 2017, mwanao anatakiwa kuwepo shuleni mwezi huo. Kutofika shule kwa wakati uliopangwa kunaweza kumpotezea nafasi yake ya masomo, kwani mwisho wa kuripoti shuleni ni mwishoni mwa mwezi July 2017.
Shule ya sekondari Mkongo ipo Mkoa wa Pwani umbali wa kilomita 168 kutoka Dar es Salaam. Kwa wanafunzi wanaotoka Mikoa ya Kusini (Lindi na Mtwara) washuke kwenye stand ya mji mdogo Kibiti. Kwa wanafunzi wanaotoka mikoa mingine wafike MBAGALA RANGI TATU –DSM, ndipo watapata magari ya moja kwa moja kuelekea Kibiti, Ikwriri, Mohoro na washuke kituo cha mabasi cha Kibiti Kuna usafiri wa NOAH mpaka kijiji cha Mkongo. Ambapo umbali wake unakadiriwa kuwa kilometa 30 kutoka Kibiti. Mwanao atapokelewa shuleni endapo atasoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata vifuatavyo **A-G.**

- **A.** Maelezo Maalum ya kujiunga na shule.
- **B.** Ada na michango mbalimbali ya shule
- **C.** Sheria Kanuni na Taratibu za shule
- **D.** Maelezo binafsi ya mwanafunzi
- **E.** Fomu ya kupimwa toka kwa Mganga (Medical Examination)
- **F.** Ahadi/Kiapo Cha Mwanafunzi
- **G.** Vitabu na vifaa vingine

Tarehe ya mwisho ya kuripoti shuleni ni tarehe……
Ni matumaini yetu kwamba mwana atasoma na kuzingatia maelekezo yote na mzazi/ mlezi utamtimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

…….
JAMES S. KESSY
MKUU WA SHULE

A: MAELEZO MAALUM YA KUJIUNGA NA SHULE

1: SARE

Mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa/mahitaji yafuatayo:.

i. Suruali mbili nyeusi.
ii. Suruali mbili damu ya mzee.
iii. Shati rangi nyeupe mikono mirefu mawili.
iv. T.shirt 2 (Fulana mbili zenye nembo ya shule) kila moja Tsh 14,000/=
v. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vya kufunika visiwe virefu (Pair mbili)
vi. Mkanda mmoja mweusi upana 1½ inchi Ngozi
vii. Soksi jozi 2 au zaidi nyeusi/Dark blue
viii. Viatu vya michezo (Raba nyeusi)
ix. Kandambili kwa ajili ya kuogea tu anaweza kuja na sandlrs pia kwa matumizi ya dharura
x. Track suit (jezi za michezo) rangi ya blue zisizo na maandishi.

2: MAHITAJI YA BWENI.

i. Godoro la futi 2½ kwa 6
ii. Shuka 3 rangi ya pink
iii. Net ya mbu 1
iv. Mto na foronya mbili rangi ya pink
v. Taulo
vi. Nguo za ndani (za kutosha Bukta ya ndani na fulana 5 na machine ya kunyolea ndevu).
vii. Ndoo moja ya lita 20 (2) lita kumi kumi.
viii. Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili
ix. Vyombo vya chakula (Sahani, Bakuli Kikombe, kijiko, chupa ya chai anaweza kuja na hot pot)1 ndogo kwa ajili ya dharura za kiafya visivyo vya plasitic.

3: MAHITAJI YA TAALUMA.

i. Picha sita (6) pps akiwa amevaa shati jeupe na rangi blue nyuma ya picha
ii. Rimu 2 kwa mwaka A4 aina ya ROTATRIM, NOPATOP AU MONDI PEKEE.
iii. Result slip ya kidato cha nne (CSEE) HALISI NA NAKALA
iv. Cheti cha kuzaliwa halisi na nakala
v. Cheti cha kumaliza kidato cha nne (Leaving Certificate). Halisi na Nakala

4: MAHITAJI A DARASANI.

i. Madaftari (counter Book) 08
ii. Kalamu/Penseli za kutosha
iii. Mkebe wa hisabati (Mathematical set)
iv. Mkasi (dissection scissor) kwa ajili ya kupasulia
v. Scientific calculator.

B: ADA NA MICHANGO MBALIMBALI

Ada na michango mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

- Fedha ya kitambulisho 5,000/=

- Fedha ya stempu 2000/= kila mwaka
- Fedha ya ulinzi 10,000/=
- Fedha ya tahadhari 10,000/=
- Fedha ya ukarabati wa samani za shule 15,000/=
- Mchango wa Tshs. 10,000/= kwa wanafunzi wanaosoma sayansi (CBG) kwa ajili ya mazoezi kwa vitendo. Na kila mwanafunzi wa SAYANSI anapaswa kuja na 25,000/= kwa ajili ya KOTI la maabala litakalopatikana/ kulipiwa shuleni.
- Mchango wa mtihani wa kujipima 10,000/=
- Mchango wa mahafali 10,000/=

JEDWALI LA AINISHO LA ADA NA MICHANGO KWA KIDATO CHA TANO

	MUHULA I	MUHULA II	JUMLA
ADA	35,000/=	35,000/=	70,000/=
MICHANGO A. TAALUMA	15,000/=	-	15,000/=
B. ULINZI	5,000/=	5,000/=	10,000/=
C. TAHADHARI	10,000/=	-	10,000/=
D. HUDUMA YA KWANZA	5,000/=	5,000/=	10,000/=
E. STAMP	1,000/=	1,000/=	2,000/=
F. KITAMBULISHO	5,000/=	-	5,000/=
G. UKARABATI WA SAMANI	15,000/=	-	15,000/=
H. BIMA YA AFYA	2,000/= au Kadi ya Bima ya Afya	-	2,000/=
I. MAHAFALI	10,000/=	-	10,000/=
J. MITIHANI YA KUJIPIMA	10,000/=	-	10,000/=
(i) Fulana 2	28,000/=	-	28,000/=
Jumla			

NB: Kwa muhula wa kwanza

i. Ada(School fees) 35,000/= ilipwe kwenye account namba **2131100051**
ii. Michango Mingine

ADA: Akaunti Namba **2131100051 (**Jina la akaunt ni **MKONGO SECONDARY SCHOOL RECURENT A/C)** na **MICHANGO MINGINE,** Akaunti Namba **2131100007 (**Jina la akaunt **MKONGO SECONDARY SCHOOL, SCHOOL FUND)**

Jina la Akaunti ni **Mkuu wa Shule Mkongo Sekondari.** Utapata huduma katika tawi lolote la Benki ya **NMB Tanzania** kuwa makini katika kuweka fedha katika akaunti za shule, fedha za ada ziwekwe kwenye akaunti ya ada tu, na michango mingine yote iwekwe kwenye akaunti ya michango na si vinginevyo. Hatutahusika na uzembe wowote wa kuchanganya malipo katika akaunti za shule. Jina la mwekaji liwe la mwanafunzi na si mzazi/mlezi. Mwanafunzi aje na **PAY SLIP** ya benki wakati wa kuripoti.

C: SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADAMU, UAMINIFU, UTII na TABIA NJEMA kwa ujumla.

Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia kauli na vitendo hivyo:

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri
2. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu na ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
3. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi
   (a) Kuvuta siagara na kutumia madawa ya kulevya
   (b) Kufuga kucha na nywele
   (c) Kufuga ndevu
   (d) Kunyoa kipara
   (e) Kumpiga mwenzake
   (f) Kutukana
   (g) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
   (h) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Heleni, Mikufu, bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali, Kofia, Kanzu, Vilemba, Suruali fupi kwa kuwa Shule hii ni ya **Serikali.**
   (i) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu
   (j) Kuvaa kaptura na kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule.
   (k) Kuvaa suruali chini ya kiuno
   (l) Kuvaa nguo za mtindo, mfano- model
4. Mwanafunzi atasimama mstari wakati wa kupata huduma
5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali
6. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa Darasani Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prep) na katika mikusanyiko yoyote mfano pared ink.
7. Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule. Hivyo Mwanafunzi:-
   A. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripo kwa mwalimu anayehusika.
   B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
   C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa
   D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shule (Roll call). Ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, Mikutano ya nyumba, Mikutano ya darasa na Maabara za shule.
8. Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na **KITAMBULISHO** kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule kama:-
9. Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu kwenda Posta, Kanisani, Msikitini, Benki, Hospitali, likizo au kwa shughuli yoyote itayomlazimu kwenda nje ya shule.
10. Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shuel wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu na atapaswa kuwa na kibali (pass) cha maandishi.
11. Mwanafunzi lazima ahudhurie prep inayoanza saa 1:30 jioni na awe kitandani kwake wakati wa kuzima taa (lights out) saa 5:00 usiku.
12. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia chakula bwenini, wala kutumia electrical heater au jiko la aina yoyote
13. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhtasari wa kikao na nakala kuwasilisha kwa Mkuu wa Shule.
14. USAFI: Mwanafunzi anawajibuka kuwa msafi kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kutaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.
15. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za shule ya Sekondari Mkongo muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati lake. **Mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi kabisa.**
16. Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu **kama laini, charger, earphone, Ipad nk.** Mwanafunzi atakaebainika kumiliki simu atarudishwa nyumbani mara moja.

17. Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.
18. **MAENEO YASIYORUHUSIWA:**
    Mwanafunzi haruhusiwi kufika/kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu.
    a) Ofisi za shule
    b) Boharia za shule
    c) Kwenye disco, ngoma, mziki au kwenye sherehe yoyote ndani na nje ys shule
    d) Maabara
    e) Baa, kilabu au mahali popote panapouzwa pombe au vileo vingine.
    f) Nyumba za wageni (Guest House)
    g) Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kuuza, kutumia ua kubeba pombe, Bangi au vileo vingine
    h) Nyumba za watumishi/ walimu

MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

1. Wizi
2. Uesherati, ushoga na ulawiti
3. Ulevi wa aina yoyote
4. Utumiaji wa madawa ya kulevya
5. Uvutaji wa sigara na bangi
6. Makosa ya jinai
7. Kuoa au kuoewa
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
9. Kupigana au kumpiga mwingine
10. Kudharau Bendera ya Taifa
11. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa Shule
12. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma kwa namna yoyote
13. Kutoa lugha ya matusi
14. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla
15. Kutohudhuria vipindi

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OWM – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI
SHULE YA SEKONDARI MKONGO

Phone: +255 784 227 470
+255 786 018 438

S.L.P 40,
IKWIRIRI-RUFIJI,
TANZANIA

D: MAELEO BINAFSI YA MWANAFUNZI

MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi …….adm.Na…….
2. Kidato …….. Mchepuo…….. Mwaka ……..
3. Tarehe ya mwaka wa kuzaliwa ……..
4. Kabila la mwanafunzi ……..
5. Uraia wa mwanafunzi……..
6. Tarehe ya kujiunga na shule ya Sekondari Mkongo ……
7. Shule aliyotoka ya Sekondari ……
8. Masomo atakayokuja kusoma ……..
9. Kama ni mlemavu, taja aina ya ulemavu ……
10. Je unarudia kitado?..... kwa nini ……
11. Dini ya mwanafunzi…… Dhehebu ……..
12. Bweni utakalopangiwa ……..
13. Anwani ya kudumu ya mwanafunzi S.L.P ……
    Wilaya …… Mkoa ……..
    Tarafa …… Kata ……
    Kijiji ……Namba ya Nyumba ……..
    Simu ya nyumbani ……..
    Simu ya ofisini ……..

    BABA

14. Jina la Baba ……
15. Je, yu hai? ……
16. Kabila la baba ……..
17. Anwani yake ya sasa ……
18. Kazi yake ……
19. Mwajiri wake ……
20. Dini ya baba …… dhehebu ……
21. Je baba na mama wanaishi pamoja ……..
22. Simu ya baba …… ya kazini……

MAMA

23. Jina la mama……
24. Je yu hai……

25. Kabila la mama……
26. Mwajiri wake……
27. Anwani yake ya sasa……..
28. Dini ya mama……Dhehebu……
29. Kazi yake……Mwajiri wake……
30. Simu ya nyumbani……ya ofisini……..

MLEZI

31. Jina la mlezi……
32. Kabila la mlezi……
33. Uhusiano na mwanafunzi……..
34. Anuani ya sasa……
35. Kazi yake……
36. Mwajiri wake……
37. Dini ya mlezi……Dhehebu……
38. Simu ya nyumbani……ya kazini……..

NDUGU WENGINE

JINA	ANUANI	SIMU	MAHUSIANO

HABARI NYINGINE

……
……
……

SAINI

Sahihi ya mwanafunzi……..Tarehe……

Jina la mwalimu wa Darasa……

Sahihi ya mwalimu wa darasa……..Tarehe……..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OWM – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI
SHULE YA SEKONDARI MKONGO

Phone: +255 784 227 470
+255 786 018 438

S.L.P 40,
IKWIRIRI-RUFIJI,
TANZANIA

E: MEDICAL CERTIFICATE

To the medical officer ……..
……..
……..
……..

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF …….. FORM V

Please examine the above named as to his fitness for admission to school as a student.

Name and signature of requesting officer

Name …….. signature ……
Date ……..

(***To be completed by a Medical Officer)***

I have examined the above named and I consider that he is physical fit/unfit to pursue as stated above.

Name and signature of Certifying Officers.

Name …….. Signature …….
Station ……Designation ……
Date …… STAMP ……

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OWM – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI
SHULE YA SEKONDARI MKONGO

Phone: +255 784 227 470
+255 786 018 438

S.L.P 40,
IKWIRIRI-RUFIJI,
TANZANIA

F: AHADI/KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ……
Ambaye nimechaguliwa kujiunga na **SHULE YA SEKONDARI MKONGO KIDATO CHA 5** Combination ya …… mwaka 2015 ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidiii na kufikia malengo ya Taifa na Shule ya Sekondari ya Mkongo.

Ninatambua kuwa nafasi huu ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni.

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyo chaguliwa kusoma
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine ziatakzokuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumba kumwita mzazi/mlezi wangu …….. (jina la mzazi) kwa ajili ya hatua zaidi.
Saini ya mwanafunzi …… tarehe …….

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi …… ninakubali mtoto wangu …….. kupata na kupokea nafasi katika shule ya Sekondari Mkongo mwaka 2015. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa.
Anuani yangu ni ……..
……..
Simu……
Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi lazima nitaijulisha shule kwa maandishi
Saini ya mlezi/ Mzazi …… Tarehe …….

G: VITABU NA VIFAA VINGINE

JINA LA KITABU	MWANDISHI
Fundament Geography	Josephat Mwita A-M
Practical Geography for Africa	John Richard
Physical Geography	Monk House
Inorganic Chemistry	TIE
Physical Chemistry vol I & II	By Mzumbe Book Project
Biologial Science	DJ Tylot
Understanding Biology for Advanced	By Grenn & Susan
Advanced Biology Principles and Aplication	By CJ Clegg & DG Mackean

Mzazi unashauriwa kumnunulia mtoto wako vitabu kama ilivyo ainishwa ki combination hapa chini na mwanafunzi atavionyesha atakapofika kuripoti. Vifaa vya usafi ni **lazima** kwa kila mwanafunzi kama jedwali linavyoonyesha.

VIFAA VYA USAFI

1. Fagio la chelewa lenye mpini
2. Fagio la kudekia (hard broom)
3. Fyekeo (kwanja)lililonolewa